

**HOTUBA YA MHE. SAIDI M. SADIKI, MKUU WA  
MKOA WA KILIMANJARO WAKATI WA UFUNGUZI  
WA MAADHIMISHO YA UHURU WA VYOMBO VYA  
HABARI MKOANI KILIMANJARO  
TAREHE 10/05/2017**

- Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Moshi na Hai;
- Kamanda wa TAKUKURU (M) Kilimanjaro;
- Kamanda wa Polisi (M) Kilimanjaro;
- Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (M) Kilimanjaro;
- Ndg. Viongozi wa Serikali na Dini;
- Wadau wa Habari;
- Wana Habari;
- Wageni waalikwa;
- Mabibi na Mabwana:

**Bwana Yesu Asifiwe!  
Tumsifu Yesu Kristo!  
Asalam Aleikum!**

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia kukutana hapa siku ya leo. Aidha napenda kuwapongeza wana habari kupitia Club yao hapa Mkoani kwa kuandaa maadhimisho ya Uhuru wa Habari.

Ninazo taarifa kuwa maadhimisho haya yalikuwa yafanyike tarehe 03/05/2017 lakini kwa utashi wenu mmeamua kwa kauli moja kuyasogeza mbele hadi tarehe ya leo.

Kutokana na hali hiyo napenda pia kutumia nafasi hii kuwa shukuru kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika shughuli hii. **Ahsanteni sana!**

### **Ndugu Mwenyekiti;**

Katika Ulimwengu wa leo binadamu anahitaji kupata taarifa/habari za mambo mbalimbali kwa wakati na kwa usahihi wake. Aidha kutokana na teknolojia tuliyonayo katika ulimwengu wa leo, habari/taarifa zinawezekana kuwafikia watu wengi kwa wakati mmoja.

Napenda kutumia fursa hii kuwajulisha wana-habari na wadau wa habari kuwa kutokana na maendeleo ya teknolojia tuliyo nayo habari inaweza kuwa kichocheo cha **maendeleo** au **kinyume** chake. Hivyo napenda kutoa wito kwenu nyote kuhakikisha habari zinazotolewa zinalenga katika kuchochea **maendeleo, amani** na **kukemea maovu** yaliyopo katika jamii tunayoishi mathalani katika Mkoa wetu tunalo tatizo la baadhi ya wananchi kuwa na **ulevi uliokithiri, ubakaji, utumiaji wa madawa ya kulevya na uharibifu wa mazingira.**

Nitafurahi sana ninyi kama wana habari kuueleza Umma ukweli na athari za kujiingiza katika shughuli hizo.

Hakika kwa kufanya hivyo tunaweza kuleta mabadiliko chanya katika jamii yetu. Kwa kufanya hivho mnaisaidia Serikali katika vita dhidi ya Ubakaji, Ulevi, Uharibifu wa Mazingira n.k.

Aidha; habari inaweza kubomoa au kuleta vurugu katika jamii. Tunayo mifano mbalimbali hapa duniani inayo dhihirisha jinsi vyombo vya habari vilivyo weza kuleta machafuko. Majirani zetu wa Rwanda mwaka 1994, tumeshuhudia jinsi baadhi ya vyombo vya habari vilivyoweza kuchochea mauaji ya Kimbary. Tukiwa kama watanzania hatuna budi kukemea hali hiyo na vyombo vyetu vya habari vinatakiwa kuweka kipaumbele katika kutoa habari/taarifa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Nchi. Nafahamu kuwa katika Mkoa wetu tunavyo vyombo mbalimbali nitoe wito kwa vyombo hivyo kutekeleza hilo.

### **Ndugu Wana Habari;**

Kabla sijahitimisha hotuba yangu, napenda kutoa maelekezo yafuatayo:-

- (i)Wanahabari wajue kuwa hivi sasa tunatakiwa kutochanganya habari na siasa. Endapo tunachanganya habari na siasa huu ndio utakuwa mwanzo wa uvunjifu wa amani;

- (ii) Vyombo kuwa na mwelekeo wa kisiasa, uzushi na uongo, udini n.k.;
- (iii) Vyombo viepuke ushabiki;
- (iv) Wadau wa Habari wakiwemo Serikali yenyewe na Taasisi zinginezo, tunao wajibu wa kutoa ushirikiano kwa wana habari pindi wanapo hitaji habari mbalimbali kutoka katika maeneo yetu. Aidha katika hili nasisitiza kuwa habari hizo zitakazo tolewa na wadau wa habari ziwe ni zile zenye kulenga kuleta **maendeleo** na **amani** kwetu sote. Wengine hunyimwa habari kwa kuwa vina vina rekeki ya kupotosha au kuandika uongo;
- (v) Nadhani mtakubaliana nami kuwa katika Mkoa wetu tunavyo vitu vingi ambavyo watu/jamii haivijui kwa undani wake. Tunazo rasilimali mbalimbali ndani ya Mkoa ambazo zinahitaji kutangazwa vizuri ili kuongeza Utalii na hivyo kuingizia Taifa letu mapato zaidi. Kwa mfano katika eneo la Hai tunalo eneo la maji moto ambalo ni zuri sana. Natamani muende pale mkatangaze kivutio hicho na vinginevyo kwa faida ya Mkoa na Taifa kwa ujumla.
- (vi) Andikeni habari sahihi na zenye uchambuzi ulio na takwimu sahihi.

## **Ndugu Wajumbe;**

Napenda kuhitimisha kwa kuwashukuru kwa mara nyingine tena kwa ukarimu wenu kama wana Habari. Pia nawapongeza kwa maandalizi mazuri ya siku yenu ya Uhuru wa Habari.

Natumaini mtafurahia siku hii kwani hakika katika Taifa letu tunao Uhuru wa Habari na ndio maana ninyi wana Habari mpo. Uhuru wa habari usingekuwepo nanyi mngekuwa hamna kazi. Kwa mantiki hiyo napenda kutoa wito kwenu kwa mara nyingine tena kuendelea kushirikiana na Serikali yetu katika kupambana na wala Rushwa, Wahujumu Uchumi, Watumiaji na Wauzaji wa madawa ya kulevya n.k.

Lakini pia tuisahau kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vyetu vya habari katika kuchochea maendeleo yetu ili tuweze kwenda sambamba na kazi ya Serikali yetu ya awamu ya Tano.

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza!**